# Kuzuwia Unyanyasaji na Zarau zidi ya Watoto



**Mu inchi ya Marekani, watoto na vijana wote, bila kujali hali yao ya uhamiaji, wanalindwa na sheria. Hizi sheria zinalenga kulinda watoto zidi ya kutumiwa mu njiya zenye haziko halali, kulumizwa na hatari.**

**Unyanyasaji wa mtoto** ni kitendo ao ni kushindwa kutenda sawa mzazi ao mlezi yenye inasababisha mazara ya kimwili ao ya kisaikolojia kwa mtoto, na hii inatiya watoto mu hatari kubwa. Kuko aina ine za unyanyasaji:

- **Unyanyasaji wa Kimwili** – kutumia nguvu za kimwili kumuazibu mtoto, jambo yenye mara mingi inasababisha majeraha.
- **Unyanyasaji wa Maneno** – vitisho, matusi ao kumuzarau mtoto.
- **Unyanyasaji wa Kihisia** – kumuyima mtoto upendo, msaada wa kihisia ao kutomujali.
- **Unyanyasaji wa Kingono** – kunyanyasa, kugusagusa, kubaka, ao kutumia mtoto kingono kwa ajili ya kupata faida.

**Zarau** ni kushindwa kutimiza mahitaji ya msingi ya mtoto ya kimwili (kama vile mavazi, chakula ao fasi ya kuishi), kihisia, kielimu ao kiafya.

**Kama uko mzazi ao mlezi wa mtoto, hii ni maelekezo fulani ya kukusaidia kuzuwia unyanyasaji wa watoto:**

- Jifunze tabia zenye zinafaa kwa watoto kulingana na umri yao.
- Wape watoto zenye unalea malezi na mazingira yenye itawasaidia kukuwa na afya ya muzuri. Kumuyima mtoto chakula, busingizi ya kutosha busiku ao matunzo ni zarau.
- Jifunze mbinu za muzuri za malezi na za kuwaazibu watoto kwa njia yenye inafaa.
- Jitunze pia: tafuta mutu wa kuzungumuza naye, pumuzika saa yenye unahitaji, ao wasiliana na huduma za ushauri kwa wazazi.

Kuko batu benye, kutokana na kazi zao, kisheria banapashwa kuripoti shaka zozote za unyanyasaji ao zarau zidi ya watoto ku bakubwa benye banahusika. Bale batu bako amo bafanyakazi ba ustawi wa jamii, walimu, washauri wa elimu na wataalamu wa afya ya akili na bafanyakazi ba afya.

**Kwa watoto na vijana: Kama unanyanyaswa, unatendewa mabaya ao unazarauliwa, unaweza kutafuta msaada kupitia masomo yako, kituo cha polisi, kituo cha kuzimisha moto, kituo cha afya ao kwa kuzungumuza na mutu mzima mwenye unaamini. Unaweza pia kuita ku simu ku Namba ya Kitaifa ya Msaada kwa Watoto wenye wananyanyaswa (1-800-422-4453) ili kwa ajili ya msaada.**

Kama unapenda kujifunza zaidi, tembelea Kituo cha Rasilimali kwa Watoto wenye hawana Wazazi ku: ucresourcecenter.org